

MKATABA WA UPANGAJI

Mkataba huu umeanza leo tarehe.....⁰¹.....mwezi.....⁰¹.....mwaka 2024.

KATI YA

THE REGISTERED TRUSTEES OF SIBTWAIN (A.S) EDUCATION TRUST FUND wa S.L P 46395 Dar es Salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **Mpangishaji**)

NA

VAN MO COMPANY LIMITED, kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania ya S.L .P 80698 (ambaye katika mkataba huu itajulikana pia kama **Mpangaji**)

Mpangishaji ni mmiliki halali wa Plot 2523, Block B, chenye hati namba 172449 kilichopo Yombo Vituka, Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam na mpangaji kwa hiyati yake amekubali kupanga kiwanja hicho kwa ajili ya kuweka yard ya magari.

HIVYO BASI, pande zote mbili zimekubaliana kama ifuatavyo:

A. MPANGAJI ANAKUBALI HAYA YAFUATAYO;

1. Mpangaji anakubali kulipa kodi ya yard kwa gharama ya shilingi za kitanzania Milioni Mbili(TZS 2,000,000) tuu kwa mwezi.
2. Kwamba, mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miaka mitano(5) na baada ya hapo pande zote mbili watakubaliana kuhusu kuongezeana muda wa mkataba.
3. Mpangaji atamlipa mwenye nyumba kodi ya muda wa miaka miwili ambayo ni jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni Arobaini na nane.(TZS 48,000,000).Pamoja na hayo hakutakuwa na ongezeko lolote la kodi ndani ya muda wote wa mkataba huu.
4. Kwamba, mpangaji atatumia kiwanja anachopangisha kwa ajili ya shughuli za yard na matumizi mengineyo ya kampuni yake ya VAN MO. COMPANY LTD ya magari tu na si vinginevyo.
5. Kwamba, mpangaji hatampangisha mtu yeyote yule bila idhini /kibali cha maandishi kutoka kwa Mpangishaji na Mpangaji hatotakiwa kukataa kukitoa kibali hicho kukiwa na sababu za msingi.

6. Kwamba, mpangaji atalazimika kutunza kiwanja hicho anachopangishwa na kukiweka katika hali ya usafi wakati wote wa Mkataba huu na endapo mkataba wake ukiisha, atalazimika kukiacha kiwanja hicho katika hali nzuri.

B. MPANGISHAJI ANAKUBALI HAYA YAFUATAYO;

1. Kwamba, mpangishaji hatombughudhi Mpangaji wakati wote wa mkataba huu iwapo Mpangaji atalipa kodi na kutekeleza masharti ya Mkataba huu.
2. Kwamba, iwapo kama Mpangishaji au Mpangaji atataka kusitisha Mkataba huu, itampasa atoe taarifa ya miezi mitatu (siku 90) kwa upande mwingine.
3. Kwamba, endapo mpangishaji atataka kuuza eneo hilo, atalazimika kumjulisha mpangaji kama mnunuzi wa kwanza, pia atampa muda maalum wa kulipa, kama mpangaji atashindwa kulipa gharama hizo basi mpangishaji atamuuzia mtu mwingine.
4. Kamba endapo Mpangaji atakiuka masharti ya mkataba huu, Mpangishaji atalazimika kuchukua hatua za kisheria baada ya mazungumzo ya Amani kushindikana.
5. Mkataba huu utatafsiriwa kwa sheria za Jamhuri ya Muungano Tanzania.

KWA KUSHUHUDIA HAYA YOTE, Mpangishaji na Mpangaji wameweka sahihi zao siku na tarehe kama ilivyo oneshwa hapa chini.


IMESAINIWA NA KUGONGWA MHURI hapa
Dar es Salaam na **THE REGISTERED TRUSTEES
OF SIBTWAIN (A.S) EDUCATION TRUST FUND**

Ambaye ninamfahamu mimi binafsi leo.....
mwezi, 01 2024

Jina: MAJID JUMA NISHAJA
Sahihi: Mtambaji
Wadhifa: MTAMBAJI Mkuu (CEO)



IMESAINIWA NA KUGONGWA MHURI hapa
Dar es Salaam na **VAN MO COMPANY LTD**
Ambaye ninamfahamu mimi binafsi leo.....
mwezi, 2024



Jina:
Sahihi:.....
Wadhifa:.....

MBELE YANGU:

Jina: ... LETICIA P. Msechu
Sahihi: ... [Signature]
Wadhifa: ... WAKILI

